

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAAA
JIMBO KATOLIKI MAHENGE – KAKWIRE CO – OPERATION
MUONGOZO WA USAHISHAJI SEPTEMBER, 2019
KIDATO CHA PILI

021

KISWAHILI

swali 1

i	ii	iii	iv	v	vi	vii	viii	ix
D	C	B	C	A	D	C	B	A

(x) mafunzo tunayoyapata kwa mama yana faida ya watu wengine yanalenga kuharibu. (alama 10)

swali la 2

- i) Azingatie kichwa cha fipisho.(kichwa cha habari cha weza kuwa tofauti tofauti)
- ii) Mwanafunzi aandike kwa aya mbalimbali
- iii) Azingatie alama za uandishi
- iv) Asikopi habari bali atumia maneno yake bila kupoteza maana ya awali ya habari
- v) mwanafunzi azingatie idadi za maneno (alama 5)

swali la 3(a)

- i. ean-----kiambishi tamati cha kauli ya kutendeanana
- ii. ye----- kiambishi awali kirejeshi
- iii. Ha-----kiambishi awali kikanushi
- iv. ek-----kiambishi tamati kauli ya kutendeka
- v. me----- kiambishi awali njeo,wakati timilifu (alama 5)

(b)(alama 7.5)

NENO	VIAMBISHI AWALI	KIINI	VIAMBISHI TAMATI
i) Amenyweshwa	a-me-	nyw	-esh-a
ii) Wamekula	Wa-me-	-kul-	-a
iii) Amekuja	a-me-	-kuj-	-a
iv) Salishana		Salish-	-an-a
v) Wamesomeana	Wa-me-	-som-	-ean-a

Swali la 4.

- i. E
- ii. W+V
- iii. T
- iv. E
- v. t (*alama 2.5*)

swali la 5(a)

- I. Ni jinsi ya kutumia lugha kwa kuzingatia mila na desturi/kaida za lugha husika. (*alama 1*)
- II. -Mada ya mazungumzo

-Uhusiano baina ya wahusika

-Lengo la mazungumzo

-Mandhari au mazingira ya kutendea (*alama 4*)

5(b)

- Kaka amenipiga picha
- Kaka amebeba picha yangu
- Amenifanania

- Dada alinichagua
- Dada alipiga kura kwaniaba yangu

- Tulishauriwa kwenda sehemu yenye mwinuko(kilimani)
- Tulishauriwa kuotesha mbengu kilimani

- Nipe sahali iliyoko upande wa kulia
- Chombo cha kuwekea chakula

- Mpikie mwanangu
- Pika kwa niaba (*alama 5*)

swali la 6(a)

- i. Huzuka na kutoweka
- ii. Ni lugha isiyo sanifu ambayo huzushwa na watu we nyetamduni moja ili kukidhi haja ya mawasiliano
- iii. Misimu iinaweza kubeba chuki ,kebehi,na utani ambao unaweza kusababisha kutoelewana katika jamii
- iv. Ni lugha iliyojaa matumizi ya balagha,yaan ni lugha yenye chumvi nyingi
- v. Misimu ni lugha ya mafumbo makubwa hivyo hueleweka na watu wachache tu. (*alama 5*)

(b)

- i. Kusoma ni muhimu hivyo hatuna budi kutilia mkazo(kisarufi/maumbo)
- ii. Siku hizi bidhaa ni ghali sana(kisarufi/kimatamshi)
- iii. Mtoto angelipelekwa hospitalini angelipona (kisarufi/muundo)
- iv. Mzee Nasoro ana ukata mno hivyo uwezo wa kununua gari hana (kisarufi/kimaumbo)
- v. Mimi nimekaa sana kwa nia (kwa ajili)ya kukungoja wewe (kisarufi)(alama 5)

swali la 7

- (a) Mwanafunzi ataje njia tatu za uhifadhi wa kazi za fasihi simulizi pamoja na hoja moja kwa kila ubora na udhaifu (alama 5)

NJIA	UBORA	UDHAIFU
1.KICHWANI	-huweza kurithishwa kizazi kimoja na kingine	-kumbukumbu kupungua
2.MAANDISHI	-hudumu kwa muda mrefu	-haitaambatana na matendo ya wahusika
3.KANDA ZA VIDEO ,FILAMU NA TELEVISHENI	-huweza kurekodi sura na sauti	-wanaofaidi ni wachache wenye uwezo wa kununua au kuvipta vitu hivyo

(b)

- i. Fanani(mtambaji/msimulizi)
- ii. Hadhira(watazamaji)
- iii. Wanyama(viumbe hai)
- iv. Vitu na mahali(jiwe,makaburini,mkuki,kichakani,kanisani)
- v. Bindamu.(alama 5)

swali la 8

- i. MIVIGA
Ni sherehe zinazofanika katika kipindi maalumu cha mwaka(jando na unyago kutawazwa wa chifu)
- ii. VICHEKESHO
Ni maigizo mafupi yenye lengo la kufurahisha na kuchekesha hadhira.
- iii. MAJIGAMBO
Ni ile hali ya kujitamba kwa mtu akijihusisha na maonesho huku akifanya mambo mbalimbali kujionesha kuwa yeye ni wa maana au shujaa
- iv. NGONJERA
Ni mazungumzo yenye muundo wa majibizano baina ya pande mbili au zaidi na baadaye hufikia makubaliano.
- v. MICHEZO YA KUIGIZA
huigiza matukio mbalimbali ya maisha ya jamii fulani. (alama 10)

swali la 9(a)

- i. Ana mkono mrefu
- ii. Ana mkono wa birika
- iii. Aमेvaa miwani
- iv. Asi ukapera/amepata jiko
- v. Amezunguka mbuyu(*alama 5*)

(b)- Ina hali ya utendaji

-Fanani na hadhira hushirikiana

-Huzaliwa,hukua,huishi,hufa

-Ni mali ya jamii nzima mtunzi hajulikani

-Huenda na wakati na mazingira (*alama5*)

swali 10.(a)

- i. Jina la mtu anayeandika
- ii. Jina la mwalikwa
- iii. Madhumuni ya mwaliko
- iv. Tarehe ya tukio na muda wa kuanza
- v. Mahali itakapofanyikia
- vi. Mawasiliano(*alama 5*)

(b)Mwanafunzi azingatie mambo ya kuzingatia katika uandishi wa kadi ya mwaliko.

(*alama 10*)